JIFUNZE KUSWALI KAMA ALIVYOSWALI MTUME WETU [ﷺ]

Mwandishi:
Abū Raslān Mūsā Kilongozi

Alisema Mtume (ﷺ):

"صَلُّوا كَمَا رَأَيْتُمُونِي أُصَلِّي"

SWALINI KAMA MLIVYONIONA NIKISWALI.

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين.

Sifa njema zote ni zake Allah Mola wa walimwengu, Swala na Salamu ziwe juu ya Mtume wetu Muḥammad (ﷺ) na Watu wake na Maswahaba zake wote.

Ama baada ya hayo;

Hii ni risala kuhusu mafundisho ya kutekeleza ibada tukufu ya swala kama alivyoitekeleza Mtume wetu (ﷺ). Risala hii nimeifupiza sana ili kila muislamu anayehitaji kuijua ibada hii, hata yule wa kiwango cha chini kabisa katika elimu, apate kufaidika. Na kwa kuzingatia kuwa yapo mas'ala yenye ikhtilafu ndani yake, nimetosheka na kutaja yale niliyoyaona kuwa ni yenye kuafikiana na dalili sahihi.

Na katika kuandika ujumbe huu, nimeegemea kwenye risala mbili tu: *"Talkhīsw swifati swalāti-n-Nabiyy"* ya Shaykh Muḥammad Nāswiruddīn al-Albāniyy (Allah amrehemu), Pamoja na *"Manhaju-s-Sālikīn"* ya Shaykh 'Abdu-r-Raḥmān Nāswir as-Sa`adiyy (Allah amrehemu).

YALIYOMO KATIKA RISALA HII:

- Maana ya Swala
- Fadhila za Swala
- Hukumu ya mwenye kuacha Swala
- Namna ya kuswali hatua kwa hatua.
- Baadhi ya makosa wanayoyafanya wengi ndani ya swala.

❋ ❋ ❋

I. MAANA YA SWALA

Swala maana yake:

- Kilugha ni: Dua.
- Kisheria ni: Ibada yenye kauli na vitendo makhsusi, yenye kufunguliwa kwa *Takbīrah* na kufungwa kwa *Taslīm*.

II. FADHILA ZA SWALA

Hakika swala ina nafasi kubwa katika Uislamu, na fadhila zake ni nyingi mno kama ilivyobainishwa katika Kitabu cha Allah na Hadithi za Mtume wake (ﷺ). Tutataja baadhi ya fadhila zake kwa ufupi:

- ✓ Swala ni nguzo ya pili katika nguzo tano za dini. Kwa utukufu wake, ndiyo yenye kufuata baada ya shahada mbili.

- ✓ Imefaradhishwa juu ya umma huu usiku wa Mi'rāj kabla ya Hijrah kwa miaka mitatu takriba.

- ✓ Tofauti na ibada zingine, swala amepewa nayo Mtume (ﷺ) akiwa mbinguni na ameipokea moja kwa moja kutoka kwa Mola wake bila ya kupitishwa kwa Jibrīl (عليه السلام).

- ✓ Mwenye kusimamisha swala hunyanyuliwa na kuwa katika daraja za juu kabisa pia swala ni sababu ya kuingia peponi na kuwa pembezoni (karibu) na Mtume (ﷺ).

- ✓ Swala uwajibu wake hauanguki katika hali yoyote ile. Kila mwislamu aliyekwisha baleghe, ni wajibu juu yake kuisimamisha katika hali yoyote ile atakayokuwa nayo; ni mamoja akawa mkaazi wa mji au msafiri, mwenye afya nzuri au mgonjwa, mwenye kuwa katika hali ya usalama na amani au mwenye kuwa katika hali ya khofu na vita. Mwenye udhuru ataitekeleza kulingana na hali aliyo nayo kadri ya uwezo wake.

- ✓ Ndio jambo la kwanza atalohesabiwa kwalo mja siku ya Qiyāmah katika matendo yake. Siku hiyo, ameneemeka na kufaulu ambaye swala yake itakuwa nzuri yenye kukubaliwa, na ameangamia na kula hasara ambaye swala yake itakuwa mbaya yenye kukataliwa.

- ✓ Ni Ibada katika ibada zilizo kubwa, ndani yake imekusanya mambo mengi matukufu, mfano: Kusoma Qur-ān, Takbīrah, Tasbīḥ, Taḥmīd, Kumsalia Mtume (ﷺ), Kisimamo, Rukū'u, Sujūd, Dua, …

- ✓ Inakataza machafu na maovu, kwa maana yule mwenye kuitekeleza anakuwa ni mwenye kujiweka mbali na mambo maovu, machafu na madhambi.

- ✓ Mfano wake mtu mwenye kusimamisha swala tano, Allah anavyomfutia kwazo madhambi yake, ni kama mfano wa mtu anayeoga kila siku mara tano ndani ya mto unaopita mbele ya nyumba yake; mtu huyo haiwezekani kubaki na uchafu kwenye mwili wake. Hivyo ndivyo mwenye kutekeleza vizuri swala tano husafika na madhambi.

- ✓ Mtu akiswali, basi atafutiwa makosa aliyoyafanya baina ya swala hiyo na ya kabla yake ikiwa atajiepusha na madhambi makubwa makubwa.

- ✓ Mtu anapoelekea msikitini kwa ajili ya swala, kwa kila hatua anayoipiga ataandikiwa mema na kupandishwa daraja nyingi.

- ✓ Malaika wataendelea kumuombea dua mwenye kuswali hata baada ya swala muda wa kuwa pahala pale alipofanyia ibada.

III. HUKUMU YA MWENYE KUACHA SWALA

- Mwenye kuacha swala, akaikanusha na kupinga uwajibu wake, huyu kisheria ni kafiri. Uwajibu wa swala ni katika mambo ya lazima kwa kila muislamu kuyajua. Hakuna ikhtilafu baina ya wanachuoni juu ya ukafiri wa mwenye kupinga uwajibu wa swala, bali wote wamekubaliana juu ya hilo; mwenye kupinga uwajibu wa swala anakufuru hata kama ataswali.

- Ama mwenye kuacha swala kwa uzembe au uvivu hali ya kuwa anakubali uwajibu wake, huyu ndiye juu ya hukumu yake wanachuoni wametofautiana. Kauli sahihi ni kwamba naye pia anakufuru hata kama hajakanusha uwajibu wake, ni mamoja akizembea na kuacha swala moja au mbili tu au akaiacha ijumaa mpaka ijumaa.

IV. NAMNA YA KUSWALI

1. Unapotaka kuswali, kabla ya kuanza kabisa, hakikisha mwili wako ni msafi kutokamana na hadathi kubwa au hadathi ndogo. Hakikisha pia usafi wa nguo na sehemu ya kuswalia kutokamana na najisi.

2. Ni lazima uchukue udhu kama alivyofundisha Mtume (ﷺ) na wakafanya hivyo Maswahaba zake (Allah awaridhie).

3. Yakupasa baada ya hayo uelekee Qiblah (al-Ka'bah/Makkah) katika swala zako za aina yoyote ile.

4. Ni wajibu kwako kusimama unaposwali swala ya faradhi, kwa maana usimame kama inavyojulikana, si kwa maana ile ya kusimama pale unapo soma kitu.

5. Baada ya kuelekea Qiblah na kusimama vizuri, ni wajibu kuleta Takbīrah kwa kusema:

ALLĀHU AKBAR (اللهُ أَكْبَرُ)

Hii inaitwa Takbīratul-iḥrām. Wakati wa kuitoa, utainyanyua mikono usawa wa mabega au usawa wa masikio bila ya kugusisha vidole gumba kwenye njewe za masikio.

6. Kisha utauweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto na yote miwili ikiwa juu ya kifua chako, na wala usiweke mikono yako kwenye tumbo au juu ya kitovu.

7. Na ni juu yako kuwa na utulivu ndani ya swala, na uangalie mahala pa kusujudia tu pasina kutizama kuliani wala kushotoni mwako, pasina kuinua macho yako juu wala kuzungusha shingo lako.

8. Kisha baada ya Takbīratul-iḥrām, utasoma dua ya ufunguzi:

"اللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ، اللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنْ خَطَايَايَ كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ، اللَّهُمَّ اغْسِلْنِي مِنْ خَطَايَايَ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ"

(ALLĀHUMMA BĀ‘ID BAYNĪ WA BAYNA KHATWĀYĀYA KAMĀ BĀ‘ADTA BAYNAL-MASHRIQ WAL-MAGHRIB, ALLĀHUMMA NAQQINĪ MIN KHATWĀYĀYA KAMĀ YUNAQQĀ-TH-THAWBUL-ABYADWU MINA-D-DANASI, ALLĀHUMMA-GHSILNĪ MIN KHATWĀYĀYA BIL MĀI WATHTHALJ WAL-BARAD).

9. Baada ya dua ya ufunguzi, utasoma:

"أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ"

(A’ŪDHU BILLĀHI MINA-SH-SHAYTWĀNI-R-RAJĪM)

"بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ"

(BISMILLĀHI-R-RAḤMĀNI-R-RAḤĪM)

Utasoma kwa ukimya pamoja na kutikisa midomo, sawa katika swala za kimya au swala za wazi, usiisome basmalah kwa sauti.

10. Kisha utasoma sūratul-Fātiḥah kwa ukamilifu na kwa hukumu zake bila kubadilisha maana yake wala kugeuza herufi zake. Na sūratul-Fātiḥah ni wajibu kuisoma katika kila rakaa hata ukiwa unaswali nyuma ya imamu. Kisha baada ya hapo utasoma sura nyingine.

11. Kuhusu usomaji wa Qur-ān kwa sauti au kwa ukimya:

- Ikiwa we ni imamu au unaswali pekee yako, utaisoma sūratul-Fātiḥah na sūra nyingine baada yake kwa sauti katika rakaa mbili za swala ya Fajr pia katika rakaa mbili za kwanza za swala ya Maghrib na rakaa mbili za kwanza za swala ya ‘Ishāi, na utaisoma sūratul-Fātiḥah kwa ukimya katika rakaa zote za swala ya Dhuhr na ‘Aswr pia katika rakaa ya tatu ya swala ya Maghrib na rakaa mbili za mwisho za swala ya ‘Ishāi.

- Ama ukiwa nyuma ya imamu, utaisoma sūratul-Fātiḥah kwa ukimya katika rakaa zote za swala ya Fajr, Dhuhr, ‘Aswr, Maghrib na ‘Ishāi. Ni wajibu kwako kuisoma sūratul-Fātiḥah hata ukiwa nyuma ya imamu.

12. Baada ya kisomo utainyanyua mikono yako kama ulivyofanya katika Takbīrat-ul-iḥrām na kwenda katika Rukū‘u huku ukisema “ALLĀHU AKBAR”. Utauinamisha mgongo wako na utajitahidi kuunyoosha hadi kulingana sawa sawa bila ya kuuinua kwa mbele au kuuinamisha chini sana kwa kuviweka vitanga vyako viwili na kushikilia juu ya magoti hali ya kutenganisha baina ya vidole. Kichwa pia usikiinamishe wala usikiinue bali kiwe baina ya hali hizo mbili, na utatulia na kuusawazisha uti wa mgongo hadi kila kiungo kitulie pahala pake na uirefushe Rukū‘u yako.

13. Katika Rukū‘u utasoma maneno haya mara tatu:

"سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ"

(SUBḤĀNA RABBIYAL-‘ADHWĪM)

Wakati mwengine unaweza kusoma zaidi ya mara tatu au chini ya hapo hadi mara moja, na Adhkār za kwenye Rukū‘u zilizothibiti kutoka kwa Mtume (ﷺ) ni nyingi, niliyoitaja ni moja wapo.

14. Kisha utainuka kutoka Rukū‘u kwenda kusimama ilhali umenyanyua mikono tena, kama ulivyoinyanyua katika Takbīrat-ul-iḥrām, huku ukisema:

"سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَه"

(SAMI‘A-LLĀHU LIMAN ḤAMIDAH)

Maneno hayo utayatamka ikiwa we ni mwenye kuongoza swala au ukiwa unaswali pekee yako.

15. Halafu utalingana sawa na kutulizana katika kusimama kwako huko kisha utasema:

" رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ "

(RABBANĀ LAKA-L-ḤAMD)

16. Baada ya kisimamo hiki, utasema “ALLĀHU AKBAR” huku ukiporomoka katika Sujūd. Na utatanguliza chini mikono miwili kabla ya magoti yako.

17. Hakikisha umesujudu kwa viungo vyako saba vifuatavyo: Paji la uso na pua (hivi vinahesabika kuwa ni kimoja; ni uso), vitanga viwili vya mikono, magoti mawili na miguu miwili (bimaana ncha za mbele za nyayo mbili).

18. Katika Sujūd yako:

- utajiegemeza juu ya vitanga vya mikono yako, utavilaza chini usawa wa masikio yako au usawa wa mabega yako na utavibana pamoja vidole vyako huku ukiwa umevielekeza Qiblah,
- utaliweka paji la uso na pua lako chini,
- unyooke vizuri na wala usilaze mikono yako chini, bali utainua sehemu za chini za mikono yako zinazoanzia kwenye viwiko, na utaitanua ili kuiweka mbali na mbavu zako,
- ncha za miguu yako zinatakiwa ziguse ardhi na ziwe zimebanana wala zisiwe zimeachana.

19. Ukishatulizana vizuri katika Sujūd yako utasoma maneno haya mara tatu:

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى

(SUBḤĀNA RABBIYAL-AA'LĀ)

Wakati mwengine unaweza kusoma zaidi ya mara tatu au chini ya hapo hadi mara moja. Na adhkār za kwenye Sujūd zilizothibiti kutoka kwa Mtume (ﷺ) ni nyingi, hiyo niliyoitaja ni moja wapo.

20. Urefu wa Sujūd yako utakuwa sawa au wenye kukaribiana na urefu wa Rukū‘u yako. Ni vizuri ukithirishe dua katika Sujūd, na vizuri zaidi ni kuzisoma kwa lugha ya kiarabu na kutumia hasa hasa zile alizokuwa akizisoma Mtume wetu (ﷺ). Na haifai kusoma Qur’an katika Sujūd kama ambavyo haifai kuisoma katika Rukū‘u.

21. Kisha utainua kichwa huku ukitoa Takbīrah “ALLĀHU AKBAR” kwa ajili ya kikao cha baina ya Sujūd mbili. Na hili ni wajibu kulifanya.

22. Katika kikao hiki:

- unatakiwa kukaa kwa kunyooka na kutulizana hadi kila kiungo kitulizane mahala pake,
- mguu wako wa kushoto utaukalia kwa kuutandaza na kuweka unyayo wake chini ya makalio. Ama mguu wako wa kulia, utainua muundi wake kwa kupindisha vidole vyake na kuvielekeza Qiblah,
- viganja vyako utaviweka kwenye mapaja mwishoni juu ya magoti, na utavielekeza Qiblah vidole vyako.

23. Urefu wa kikao hiki utakuwa sawa au wenye kukaribiana na urefu wa Sujūd yako na utasoma maneno yafuatayo kwa idadi utakayoiweza:

"رَبِّ اغْفِرْ لِي رَبِّ اغْفِرْ لِي"

(RABBI-GH’FIR LĪ, RABBI-GH’FIR LĪ)

24. Halafu utatoa Takbīrah tena kwa kusema “ALLĀHU AKBAR” kwa ajili ya kuelekea kwenye Sujūd ya pili. Na utafanya kwenye Sujūd ya pili kama ulivyofanya kwenye Sujūd ya kwanza.

25. Kisha utanyanyuka kutoka katika Sujūd ya pili kwa ajili ya kutekeleza Rakaa ya pili. Utainuka kwa kuiegemea mikono yako miwili huku ukileta Takbīrah kwa kusema “ALLĀHU AKBAR”; na hutoinyanyua mikono yako.

26. Rakaa yako ya pili utaitekeleza na kufanya kama ulivyofanya katika Rakaa ya kwanza isipokuwa hutosoma dua ya ufunguzi na utaifanya Rakaa hii kuwa fupi kidogo kuliko ya kwanza.

27. Ukiimaliza rakaa hii ya pili, baada ya Sujūd yake ya pili, utakaa kikao kwa ajili ya Tashahhud; na hili unalazimika kulifanya. Utakaa kama nilivyoeleza kwenye kikao cha baina ya Sujūd mbili, na kiganja chako cha kushoto utakilaza kwa kukinyoosha kwenye goti mwishoni mwa paja la kushoto.

28. Kiganja chako kikiwa kwenye goti mwishoni mwa paja la kulia, utanyoosha kidole cha shahada huku ukitamka maneno yafuatayo kwa siri bila kunyanyua sauti:

"التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ، أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ"

(ATTAḤIYYĀTU LILLĀHI WA-SWSWALAWĀTU WA-TWTWAYYIBĀTU, ASSALĀMU ‘ALAYKA AYYUHA-NNABIYYU WARAḤMATULLĀHI WABARAKĀTUH, ASSALĀMU ‘ALAYNĀ WA ‘ALĀ ‘IBĀDI-LLAAHI-SWSWĀLIHĪNA, ASH-HADU AN-LĀ ILĀHA ILLA-LLĀHU, WA ASH-HADU ANNA MUḤAMMADAN ‘ABDUHŪ WARASŪLUHŪ).

29. Ikiwa swala hii unayoswali hapa ni swala yenye rakaa tatu au nne, basi utatosheka na kusema hivi bila ya kuongeza kitu chochote zaidi ya dua zilizothibiti kutoka kwa mtume (ﷺ).

30. Na ikiwa ni swala yenye rakaa mbili tu, basi kikao hiki kitakuwa ndiyo cha Tashahhud ya mwisho, kwa hiyo itakuwa wajibu kwako kuongeza dua ya kumswalia Mtume wetu (ﷺ) kama ifuatavyo:

"اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ"

(ALLĀHUMMA SWALLĪ ‘ALĀ MUḤAMMADIN WA ‘ALĀ ĀLI MUḤAMMADIN, KAMĀ SWALLAYTA ‘ALĀ ĀLI IBRĀHĪYMA, INNAKA ḤAMIYDUN MAJĪD. ALLĀHUMMA BĀRIK ‘ALĀ MUḤAMMADIN WA ‘ALĀ ĀLI MUḤAMMADIN, KAMĀ BĀRAKTA ‘ALĀ ĀLI IBRĀHĪMA, INNAKA ḤAMĪDUN MAJĪDUN).

31. Halafu baada ya dua hii ya kumswalia Mtume wetu (ﷺ), utasoma dua ya kujikinga na mambo manne kama ifuatavyo:

"اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ، وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ، وَمِنْ شَرِّ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ"

(ALLĀHUMMA INNĪ A‘ŪDHU BIKA MIN ‘ADHĀBI JAHANNAM, WA MIN ‘ADHĀBI-L-QABRI, WA MIN FITNATI-L-MAḤYĀ WA-L-MAMĀTI, WA MIN SHARRI FITNATI-L-MASĪḤI-DDAJJĀL)

32. Na ikiwa ni swala yenye rakaa tatu au nne, basi kwenye kikao cha Tashahhud ya pili ambayo ni ya mwisho:

- Utakaa mkao maalumu (Tawarruk) ambapo utalilaza chini paja lako la kushoto, utainua muundi wa mguu wa kulia kwa kupindisha vidole vyake na kuvielekeza Qiblah, huku mguu wa kushoto ukiwa umeulaza chini ya paja la kulia na kuufanya unyayo wa kushoto ujitokeze chini ya muundi wa kulia.
- Utasoma maneno ya Tashahhud ya kwanza yaliyo kwenye nukta nambari 28, kisha baada ya hayo utasoma dua ya kumswalia Mtume wetu (ﷺ) iliyo kwenye nukta nambari 30 pamoja na dua ya kujikinga na mambo manne iiliyo kwenye nukta nambari 31.

33. Kisha baada ya dua hizo unaweza kuomba dua yoyote uipendayo. Na zote hizi unatakiwa kuzitamka kwa lugha ya kiarabu.

34. Baada ya hayo, utageuka na kufanya Taslīm kwa kusema:

السَّلاَمُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللهِ

(ASSALĀMU ‘ALAYKUM WA RAḤMATULLĀH)

Utaanzia upande wako wa kulia, utageuza shingo lako mpaka kuonekane weupe wa shavu lako la kulia, kisha utageuka upande wa kushoto na kuleta Taslīm kwa kusema (ASSALĀMU ‘ALAYKUM WA RAḤMATULLĀH) mpaka uonekane weupe wa shavu lako la kushoto. Hata katika swala ya jeneza (hivi ndivyo inatolewa salamu).

35. Ikiwa we ni imamu, basi katika kutoa salamu, utainyanyua sauti yako. Ama ukiwa nyuma ya imamu au ukiwa unaswali pekee yako, hutoinyanyua sauti; utaitoa kwa siri.

V. BAADHI YA MAKOSA WANAYOYAFANYA WENGI NDANI YA SWALA

1. Wanaponyanyua mikono kwa ajili ya kutoa Takbīrah, utawaona wakigusisha vidole gumba kwenye masikio. Hili haujapokelewa usahihi wake, hivyo ni vyema kujiepusha nalo.

2. Wanaposimama kusali husikika wakitamka nia kwa sauti kwa kusema yafuatayo au mfano wake: “USWALLĪ FARDWA SWALĀTI-DHDHUHR ARBAA’ RAKĀ’TI LILLĀHI TAĀ’LĀ IMĀMAN; ALLĀHU AKBAR”. Hili nalo halijatoka si kwa Mwalimu wetu Mtume (ﷺ) wala kwa wanafunzi wake wabora (Allah awaridhie), bali ni katika mambo yaliyowekwa na watu tu wasiotegemewa kutunga sheria.

3. Kulirefusha sana Tamshi la Allah kiasi cha kupitiliza; mfano: wanapotoa Takbīrah ya kwenda Rukū‘u, kwenda au kutoka Sujūd.

4. Baadhi utawasikia neno “AKBAR” wakilivuta kwa kulitamka AKBĀR hadi kulitoa katika maana yake halisi.

5. Kuisoma kwa haraka sana Sūratul-Fātiḥah kiasi cha kwamba ile maana inapotea. Na sunnah ni kuisoma inavyopasa kwa utulivu na tajwīd tena kwa kuzingatia maana yake, pia ni vizuri zaidi kuisoma bila kuunganisha pamoja Āyah zake.

6. Pia katika makosa yaliyoenea kwa wengi, ni kuzitamka baadhi ya lafdhi vibaya kwa kubadilisha herufi, kosa ambalo linapelekea maana kupotea au kuleta ambayo haijakusudiwa. Mfano kwenye neno la mwisho katika Sūratul-Fātiḥah, “وَلَا الضَّالِّينَ”, badala ya herufi DWĀD (ض) utawasikia wakiitamka herufi DHWĀ (ظ).

7. Baadhi ya wenye kuswali kuvielekeza viungo vyao kwengine kinyume na Qiblah (al-Kaa`bah/Makkah), mfano: mabega, miguu miwili wakati wa kusimama, vidole vya mikono wakati wa kusujudu, nk.

8. Mtu kuacha kutoa sauti walau ya chini kwa chini kipindi anaposwali pekee yake katika swala za kudhihirisha kisomo.

9. Wakati imamu anaposoma neno la mwisho katika Sūratul-Fātiḥah "وَلَا الضَّالِّينَ" utawasikia wakisema "RABBI-GH-FIRLĪ". Hakuna katika mafundisho sahihi ya Mtume wetu (ﷺ) jambo kama hili.

10. Baadhi huongeza neno "SAYYIDINĀ" wanapofikia kumswalia Mtume (ﷺ) kwenye Tashahud ya mwisho. Hili pia ni kosa.

11. Baadhi ya watu, wanapotoa salamu utawasikia wakisema "sssss" huku wakinyanyua vichwa vyao juu kwanza na kuviteremsha chini kisha ndio wavielekeze kuliani mwao na kushotoni mwao. Haya yote si katika mafundisho ya Mtume wetu (ﷺ).

12- Pia utawaona baadhi wakinyanyua mikono yao sehemu tofauti ndani ya swala wakiashiria kuomba dua, mfano: wanapoinuka kutoka katika Rukū'u. Na pale wanapotoa salamu hukimbilia kunyanyua mikono nakuipaka kwenye uso. Hili pia ni katika makosa.

❋ ❋ ❋

HITIMISHO...

Sifa njema zote ni zake Mola Wangu ambaye amenijaalia kukamilisha ujumbe huu. Nataraji kwake kunijaalia nafasi nyingine ili niweze kuandika na mengine, kusherehesha na kuziba mianya ya yale niliyoyaacha kwa kuhofia kurefusha risala hii. Pia nina mpango wa kuandika risala zingine zinazohusiana na aḥkām za Twahara ya muislamu, Zaka na mengine; namuomba Mola wangu Mkarimu aniwafikishe, anikubalie, aninufaishe mimi na awanufaishe wengine na kazi hizi.

Mwisho kabisa, nawashukuru wote waloshirikiana nami katika kukamilisha jambo hili, Allah awazidishie elimu na ikhlāsw na awalipe kheri nyingi.

Nimeianza kazi hii siku ya Jumapili tarehe 26/04/2020M ambayo ni sawa na tarehe 03/Ramadhani/1441H, na nimeikamilisha kuiandika tu tarehe 04/05/2020M ambayo ni sawa na tarehe 11/Ramadhani/1441H.

Abū Raslān Mūsā KILONGOZI

Masjid Manyema/Barabara ya 7, DODOMA-TANZANIA